# Mtazamo wa Kushukuru.

KWARESMA 2025
Mtazamo wa Kushukuru

Kwaresma, kipindi cha kuelekea Pasaka, hutupa sisi nafasi ya kukumbuka maisha, kifo na kufufuka kwake Yesu. Kuyatazama maisha yake hapa duniani kwa maajabu na mshangao na kukaa kwa usumbufu kuhusu kujitoa kwake sadaka, ili asubuhi ya Pasaka ikifika, tuwe tayari kufurahia ufufuo.

Katika Zaburi 107:1-2 tunasoma maneno haya:

'*Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, kwa maana fadhili zake ni za milele. Na waseme hivi waliokombolewa na Bwana, wale aliowakomboa na mkono wa mtesi.*

Kwaresma hii, inakualika uchukue wimbo mwepesi wa shukrani, ili kukiri na kutafakari kuhusu wema wa Mungu. Ukiwa na tendo la makusudi la kila siku, tunatumaini utapalilia moyo wenye shukurani na wimbo utakaodumu hata baada ya kwaresma kumalizika.

Kwa sababu ya Yesu, kwa sababu ya maisha, kifo na kufufuka kwake, sisi tumekombolewa, nasi tuna hadithi ya kusimulia. Mungu wetu ni mwema, na upendo wake wadumu hata milele.

Kwaresma, ikiwa na mkao wa shukrani, naomba uione dunia kwa kioo kipya na furaha katika uzuri na baraka ambazo ni zako kwa sababu ya Yesu.

**Jumatatu:** Tengeneza kumbukumbu ya kuonekana ya wema wa Mungu kwako.

'Na wamshukuru Bwana kwa fadhili zake, na maajabu yake kwa wanadamu ' (Zaburi 107:8).

Leo, orodhesha mambo yote ambayo kwa sababu yake una shukurani. Unaweza kutaka kukusanya taarifa kwenye jagi. Au labda utengeneze bango la mawazo yako yote. Mwisho wa siku, pitia kwa kuyasoma yote uliyoorodhesha chini na tafakari kuhusu wema wa Mungu.

**Jumanne**: Fanya zoezi la shukurani katika jamii.

'Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake , vile vile kama mnavyofanya' (1 Wathesalonike 5:11).

Shirikiana na rafiki, mshirika au mwana familia na mshirikishane kile ambacho kwa leo mnashukuru. Waalike nao vile vile waseme wanashukurani kwa sababu ya nini.

**Jumatano:** Jaribu uandishi wa habari.

'Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu wote, nitayasimulia matendo yako yote ya ajabu' (Zaburi 9:1).

Leo, tenga dakika chache za kuandika habari.  Tafakari kuhusu wakati uliokupa furaha, amani au faraja katika siku nzima iliyopita. Neno la fadhili. kutoka kwa rafiki, kazi uliyoikamilisha, ombi lililojibiwa, kikombe cha chai – andika chini kile ambacho unashukuru na kwanini. Jisomee kile ulichoandika na uone jinsi Mungu alivyokubariki katika njia ndogo za maana.

Ahamisi: Mwisho wa siku tafakari.

'Hatimaye, ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema, ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo' (Wafilipi 4:8).

Tenga dakika chache kabla ya kulala ili utafakari mambo matatu yaliyokwenda vizuri leo na kwanini kwa sababu ya hayo mambo unashukuru.

Ijumaa: Shukurani kwa sababu ya wengine.

'Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo. (Wafilipi 1:3).

Leo, mfikie mtu aliye maishani mwako na umfahamishe ulivyo na shukurani kwa sababu ya uwepo, msaada na mguso wake sahihi kwako. Anaweza akawa rafiki, mwana familia, mwenzako kikazi, au hata mtu ambaye hujaongea naye kwa muda. Uwe maalum iwezekanavyo.

Jumamosi: Shukurani kwa sababu ya msalaba.

Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi' (Warumi 5:8).

Unapotafakari kuhusu maisha na safari ya Yesu kwenda msalabani katika majira haya ya Kwaresma, chukua mda upige magoti kwa shukurani. Mshukuru Yesu kwa jinsi sadaka yake inavyokugusa ndani.

Jumapili: Sabato.

Chukua muda useme asante kwake Mungu kwa wema wake kwako juma hili. Mbele zako shikilia shukurani zote ulizoziandika. Kumbuka mazungumzo uliyozungumza na wengine. Kumbuka Mungu ni nani.